



CHUO KIKUU CHA DAR ESSALAAM

TANGAZO LA MAENEKO YA KUPANGA KWA AJILI YA KUTOLEA HUDUMA KWA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) kinapenda kuutangazia umma kuwa kimetenga maeneo maalumu kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali kwa wanafunzi kama ifuatavyo:

Na.	ENEKO	KAMPASI/MAHALI	HUDUMA INAYOTAKIWA
1.	Chumba Namba 3, CoICT	Kampasi ya Kijitonyama	Steshenari na kuchapisha nyaraka n.k.
2.	Chumba Namba 5 Mabibo Shopping Complex	Hosteli za Mabibo	Saluni ya Kiume

Kwa tangazo hili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinawaalika wale wote wenye nia na wanaopenda kutoa huduma hizo kama zilivyoainishwa katika jedwali hapo juu kuomba kutoa huduma. Waombaji wafike Kurugenzi ya Mipango, Mendeleo na Uwekezaji ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam iliyopo Ofisi Namba 303 Jengo la Utawala (Cranford Pratt Building) kwa ajili ya kuchukua fomu za maombi. Waombaji watalipa Shilingi elfu kumi tu (**TZS 10,000/=**) kuitia ‘Namba ya Kumbukumbu’ ambayo inapatikana Ofisi Namba 225 kwa Mhasibu wa Kurugenzi ya Mipango, Maendeleo na Uwekezaji.

Mwisho wa kuchukua fomu na kurudisha ni siku kumi na nne (14) kutoka siku ya kwanza ya tangazo hili.

Tarehe **01 Julai 2022** itakua ni siku ya kutembelea maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kutolea huduma hizo ambapo saa 4:00 asubuhi tutakutana katika Kampasi ya Kijitonyama na saa 6:00 mchana tutakutana katika Hosteli za Mabibo.

Baada ya mchakato wa kupata watoa huduma kukamilika waombaji wote wataarifiwa juu ya matokeo hayo kwa njia ya barua.

Imetolewa na

NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO, UTAWALA

24.06.2022

Jiandae Kuhesabiwa Siku ya Jumanne tarehe 23 Agosti, 2022